Maonyesho Yanayohamishika, yaliyopangwa kuanzia 2028: **Alama – Traces – Spuren**
Urithi wa Ukoloni wa Wajerumani nchini Tanzania
Maonyesho ya kazi za sanaa za uchoraji wa kisasa kutoka Tanzania na Ujerumani

Maonyesho yanalenga kuweka si tu kumbukumbu za alama zinazothibitika za ukoloni wa Kijerumani nchini Tanzania, bali pia kuziweka bayana athari za kifikra na za kisiasa zinazodumu hadi leo—hata nchini Ujerumani. Iwapo kama huu wito utakubalika na mambo yakaenda vizuri, basi huenda sanaa ya aina kipekee kabisa inaweza kuibuka na kulishangaza soko la Kimataifa.

Wachoraji wa sanaa za kisasa kutoka Tanzania na Ujerumani wanakaribishwa kushiriki, na kushiriki ni bure. Hakuna masharti ya umri, elimu wala mitindo. Kazi za zamani zinaweza kuwasilishwa pia. Kazi moja au mbili kwa kila msanii zinaweza kuonyeshwa.

Sanaa hizo zinaweza zikanunuliwa wakati huo huo wa maonyesho, ingawa malipo halisi na makabidhiano yanafaa kufanyika mara tu baada ya mfululizo wa maonyesho kukamilika. Msanii atapokea bei ya ununuzi - ukiondoa ada ya kudumu ya €150 ya kugharamia usafiri, utengenezaji wa fremu, na gharama za uendeshaji. Aidha, pia asilimia 10 (10%) ya bei ya mauzo hukatwa kwa ajili ya gharama za PR. Gharama za uhamisho zitalipwa na msanii. Wakati wa maonyesho, nakala za ukubwa wa A2 zitauzwa, huku wasanii wakipokea asilimia 50 (50%) ya bei ya mauzo. Kwa sheria na masharti, tafadhali rejea pia tanzaniart.de -> conditions.

Kazi za sanaa zinapaswa kuundwa kwenye turubai (canvas) na kusafirishwa zikiwa zimekunjwa hadi kufika Dar es Salaam au Celle - Ujerumani (linganisha tanzaniart.de -> contact). Ukubwa unaopendekezwa ni ule wenye kipimo kisichozidi sentimita 100 kwa upande mfupi na kisichopungua sentimita 50 kwa 50.

Mfano wa mada zinazoweza kujumuishwa:

Uamuzi kutoka nje / Kutawaliwa kifikra na nje: Hali ya maamuzi yako kuendeshwa na watu au nguvu za nje badala ya uhuru wako.
Dhamira / Utume: Lengo kuu au kazi maalum ambayo mtu au kundi limekusudia kuifanya.
Ubaguzi wa rangi / Utawala au ubora wa weupe: Imani au mfumo unaoweka watu weupe au rangi fulani juu ya wengine.
Mtazamo / Hali ya akili / Fikra: Jinsi mtu au jamii inavyofikiri na kuona mambo.
Hadithi za uongo / Imani potofu : Imani au mawazo ya zamani ambayo si ya kweli lakini yanaaminiwa na wengi.
Utawala wa kidhalimu / Ukandamizaji / Hofu: Mfumo wa kutawala kwa kuvunja sheria, kudhulumu watu, na kuleta woga.
Ukandamizaji wa upinzani - Jinsi watawala wa kikoloni walivyozima na kuadhibu mapambano ya wananchi waliotetea ardhi yao.
Mafanikio ya kabla ya ukoloni - Maendeleo, mifumo ya kijamii, na teknolojia iliyokuwepo barani Afrika kabla ya kuja kwa wazungu.
Utegemezi wa kudumu, kampuni - Uhusiano wa kiuchumi na biashara ambapo nchi changa bado zinategemea kampuni na mataifa ya nje.
Vielelezo au mashujaa wa baada ya ukoloni - Viongozi, mashujaa, au taasisi zilizotoa mwelekeo mzuri baada ya nchi kupata uhuru.
Majengo (shule, hospitali, maboma) - Miundombinu iliyojengwa na wakoloni kwa ajili ya utawala na huduma zao.
Magonjwa ya mlipuko - Maradhi makali yaliyoikumba jamii wakati wa mabadiliko au kuwasili kwa wageni.
Maeneo ya kumbukumbu; miti ya kunyongea - Maeneo ya kumbukumbu za kihistoria na miti iliyotumiwa kuwaua wapiganaji wa uhuru.
Majina ya mitaa, undugu wa miji - Majina ya barabara yaliyorithiwa kutokakoloni na uhusiano wa ushirikiano kati ya miji ya hapa na nje.
Miundombinu, Malezi ya watoto, Elimu na kupeleka watoto mbali: Jinsi shule zilivyobadilisha maisha ya familia.
Uchumi wa fedha na kodi: Kulazimishwa kulipa kodi kwa pesa taslimu.
Nyakati na ratiba za kila siku: Kazi za kila siku kufuata saa na sio jua.
Kazi za lazima: Watu walivyolazimishwa kufanya kazi bila hiyari.
Mazao ya ukoloni: Kahawa, pamba, na mkonge vilivyobadilisha kilimo.
Mwisho wa utumwa: Je, utumwa uliisha kweli au ulibadilika sura.

Chukua hatua ya kuanza kushiriki! Kazi zilizopo: Tuma picha pamoja na vipimo vyake! Kazi mpya: Wasiliana na mtunza maonyesho!

Fritz Gleiss, **fritzgleiss@yahoo.com**